HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 06 Januari - Aprili 2008

# Ubinafsishaji wa Baoanuai wapingwa




*Aina ya mabango yanayohamasisha wazo la Hifadhi katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa*

## NUKUU YA TOLEO

Kama tumeamua kuumia kwa ajili ya wananchi na kutetea haki zetu hakuna kitakachoshindikana ... "Nyerere alikuwa mwenyewe, mkombozi, leo mbona sisi tuko wengi, hoja ni mbinu, si wingi, si pesa!"...

*Martha Sumaye-Hanang'*

**KUMEKUWA na taarifa nyingi, malalamiko mengi yanayoonyesha kuwa uvunaji wa maliasili ya Tanzania hauna manufaa yoyote kwa wananchi walio wengi na zaidi ya hapo unawasababishia madhara makubwa watu wa kawaida hususan wale waishio jirani na maeneo ambako rasilimali hizo huvunwa na kusafirishwa nje ya nchi, na kwa kiasi fulani katika maeneo ya mijini. *Mtafiti Ng'wanza Kamata anachambua zaidi katika makala ifuatayo***

KATIKA miaka ya hivi karibuni, Wa-Tanzania wameshuhudia jinsi rasilimali za nchi ikiwemo maliasili hususan itokanayo na misitu ikiporwa na kuiacha nchi ikiwa hoi. Kumekuwa na taarifa nyingi, malalamiko mengi yanayoonyesha kuwa uvunaji wa maliasili ya Tanzania hauna manufaa yoyote kwa wananchi walio wengi na zaidi ya hapo unawasababishia madhara makubwa watu wa kawaida hususan wale waishio jirani na maeneo ambako rasilimali hizo huvunwa na kusafirishwa nje ya nchi, na kwa kiasi

Endelea Uk.3

## YALIYOMO

- Tahariri Uk.2
- Bunga bongo- Nishati Uoto Uk. 4 na 8
- Uporaji wa rasilimali za masikini Uk. 6-7
- Maoni Uk. 7
- Hifadhi ya Mali asili Bahari Uk. 9 na 11
- Kona ya Sheria, Uk. 10
- Machapisho Uk. 12

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapishaji**
Alice Shamge

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

Email:
**ecoprint@bol.co.tz**

# TAHARIRI

WAKATI mjadala kuhusu ubinafsishaji wa mali zilizokuwa chini ya mashirika ya umma au serikali ulipoanza takribani miongo miwili na nusu iliyopita, hoja tatu kubwa zilijitokeza miongoni mwa wanaharakati wa maendeleo. Wapo wale waliokuwa wakihoji mantiki nzima ya kubinafsisha mashirika hayo, wapo waliokubali yabinafsishwe lakini wakahoji namna yalivyokuwa yakibinafsishwa na kundi jingine lilishabikia ubinafsishaji kwa kwa sababu mbalimbali walizotoa. Mjadala huo tulishaufanya katika toleo mojawapo la jarida hili na si vema tukarudia maana kuna masuala tele ya kuyajadili. Lakini labda hoja moja katika hizo tatu ni muhimu tukairejea hasa kutokana na umuhimu wake kwa yale ambayo yameendelea kutendeka siku hadi siku katika kuamua mfumo wa usimamizi na matumizi ya rasilimali mbalimbali za nchi yetu.. Na hili linahusiana na namna serikali na wa-Tanzania wachache waliopewa dhamana ya usimamizi wa rasilimali hizo wanavyotekeleza majukumu yao kwa niaba ya wa-Tanzania wote na hatimaye kuleta tija au hasara kubwa katika mfumo wa maisha ya wananchi wa kawaida.

Katika jarida hili, mna taarifa za utafiti unaoonyesha jinsi rasilimali nyingi za baoanuai zinavyopotea na kuwanufaisha wachache kutokana na sababu mbalimbali kubwa ikiwa kukosekana kwa mfumo madhubuti wa usimamizi na udhibiti wa uvunaji na matumizi yake. Rasilimali hizo ni pamoja na maarifa ya asili juu ya thamani za kitiba za mimea, miti na mazao yake kama vile mizizi, magogo na maua na viumbe hai wengine kama wanyamapori na wadudu. Taarifa hizi za kitafiti zinaonyesha kuwa serikali inatilia mkazo zaidi uhifadhi wa baoanuai kwa madai ya kulinda mazingira na uoto asilia kwa vizazi vijavyo huku milango ya nyuma ikifunguliwa kwa wageni na wenye mitaji mikubwa ya kibiashara kufaidi. Cha kusikitisha zaidi ni pale jamii za maeneo yenye rasilimali hizo zinapondelea kubaki maskini katikati ya utajiri ambao ama umehifadhiwa au kuruhusiwa kwa wachache kwa minajili ya kibiashara.

Habari kwamba uvunaji wa magogo umepigwa marufuku si ngeni masikioni mwetu, lakini pia si jambo geni kusikia na hata kuona magogo yamekamatwa yakisafirishwa kwenda Uchina na kwingineko. Hapa ndipo pa kujiuliza kama uvunaji umezuiliwa, magogo yanayokamatwa yanatoka wapi, ni ya nani, yamepitaje huko kote hadi kufika bandarini wakati maafisa maliasili wapo?. Ukiacha hilo, suala la madini kutowanufaisha wazalendo na hata taifa kwa ujumla limejadiliwa sana na pengine tumaini pekee limebaki katika mapendekezo ya kamati iliyoundwa na Rais kuangalia mfumo mzima wa sekta ya madini. Hili tunaweza kuliacha kwa sasa. Lakini zipo taarifa juu ya wanyamapori kuwindwa kinyume na taratibu hasa katika mapori tengefu ya wilaya za kaskazini kama Ngorongoro na Serengeti na taarifa hizi pia zinajulikana. Ukiacha undani wa taarifa hizo, utafiti umeibua mengi pia juu ya rasilimali za baoanuai kwenye fukwe za bahari na mito zinavyotoweka na au kumilikiwa na wageni hasa maeneo ya visiwa vya Mafia na kando ya mto Rufiji huku wenyeji wakizuiliwa kupata hata samaki wa kitoweo au kutumia fukwe hizo. Na pengine, litakuwa la mshangao kwa wengi kusikia pia wadudu kama vipepeo, majongoo na hata mimea yenye asili ya kipekee hapa nchini, vinatoweka kwa kasi ya ajabu bila hatua za msingi kudhibiti hali hiyo kuchukuliwa. Mfano hai unahusu mmea maarufu unaopatikana milima ya Usambara pekee duniani Impatience Usambarensis ambao utafiti umebaini kuwa umepewa hakimiliki ya bustani moja ya Uingereza (Royal Botanical Garden) bila kufahamika kwa wenyeji wa Usambara wala kuwepo mikataba ya kibiashara kuwanufaisha wa-Tanzania.

Hali hii ya kutojali namna mali na rasilimali za wa-Tanzania zinavyovumwa na kuwanufaisha wa-Tanzania inahitaji kukomeshwa. Si wakati tena wa kuambiwa mijadala imefungwa tukanyamaza kama ilivyokuwa kwa awamu ya tatu ya uongozi wa nchi. Tumeshaona, tumejifunza vya kutosha makosa haya na hatuna budi sasa kuchukua hatua, kwanza kwa kuwawajibisha waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali hizo na pili kuchochea na kushinikiza mabadiliko katika mfumo wa sera na sheria zenye mianya ya kutoroshea rasilimali za wa-Tanzania bila wao kunufaika nazo. Hayo yanawezekana tu kwa kuibua na kuendeleza mijadala miongoni mwa wananchi wenye uzalendo wakiungwa mkono na wanaharakati wa maendeleo katika nyanja zote. Ni kwa njia hizo tu tunaweza kukabiliana na umaskini uliokithiri miongoni mwa wanachi kwani rasilimali zao zitatumika kwa ajili ya manufaa yao. Haya shime wazalendo tuungane kwa vitendo maana hakuna lisilowezekana penye nia thabiti.

# Ubinafsishaji wa Baoanuai

Inatoka uk. 1



ng'wanza kamata

fulani katika maeneo ya mijini. Kumekuwa na taarifa za ukataji na usafirishaji wa magogo nje ya nchi, uvuvi usiozingatia taratibu za uvuvi endelevu, uvunaji wa wanyamapori unaopendelea wageni na wa-Tanzania wachache ambao wanashiriki katika kutoa upendeleo huo kwa wageni. Aidha toka miaka ya 1990 wananchi wa sehemu mbalimbali wamekuwa wakilalamika namna rasilimali nyingine kama vile madini ambavyo yamekuwa yakiporwa na kufaidisha wageni dhidi ya wa-Tanzania.

Pamoja na kelele hizo, kumekuwa pia na jitihada mbalimbali za kuhifadhi maliasili na baoanuai zake. Usimamizi, uvunaji, na uendelezaji wa maliasili hizi kama ilivyo katika misitu na madini, umekuwa na mapungufu makubwa. Matokeo yake rasilimali hizi pia sio tu zinapotea lakini pia kupotea kwake hakutokani haswa na kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania bali wageni na hususan wale wenye manufaa ya kujilimbikizia mali kwa njia mbalimbali. Katika utafiti uliofanyika juu ya usimamizi, uhifadhi, na uvunaji wa baoanuai hapa nchini, wananchi mbalimbali hususan wale waishio katika maeneo yanayozunguka hifadhi zenye utajiri mkubwa wa baoanuai (kama wale wa Misitu ya Tao la Mashariki na Kazimzumbwi) walitoa mitazamo yao juu ya masuala hayo. Ufuatao ni muhtasari wa baadhi ya maoni yaliyotolewa na watu mbalimbali waliotoa maoni yao katika utafiti huo.

### Je wanavifahamu Vyombo au Mamlaka Inayosimamia Maliasili?

Sehemu kubwa ya watu waliohojiwa walionyesha kuwa na uelewa mkubwa wa vyombo mbalimbali vinavyosimamia maliasili. Mathalani asilimia zaidi ya 57 ya waliotoa majibu juu ya swali la kama wanaelewa ni chombo au mamlaka ipi inasimamia maliasili kama vile misitu na baoanuai nyingine, walitaja Wizara ya Maliasili na Utalii (44.6%) na maafisa maliasili (13.3%). Wasimamizi wengine waliobainishwa katika taarifa zilizopatikana ni mamlaka za hifadhi (14.5%), Serikali za vijiji (19.3%), makampuni binafsi (1.2%), na wengineo (3.6). Kwa mujibu wa maoni haya sehemu kubwa ya wasimamizi wa mali asili hapa nchini ni vyombo au mamlaka za serikali ambazo kwa jumla ni kama asilimia 72.3, ukiondoa serikali za vijiji.



*Moja ya maeneo katika hifadhi ya Amani*

### Je Wanaridhishwa na Taratibu za Usimamizi wa Maliasili na Baoanuai?

Kiasi kidogo tu cha asilimia 27.2 ndicho kinachoeleza kuridhishwa na taratibu za kusimamaia uhifadhi na uvunaji wa maliasili na baoanuai katika maeneo ziliko. Kiasi cha asilimia 62.9 hakiridhiki sana na taratibu zilizopo. Kutoridhika huku kunatokana na mambo mengi baadhi yakiwa kuzuiwa au kupata usumbufu mkubwa pale wanapotaka kuvuna maliasili kwa ajili ya matumizi yao mbalimbali hasa yale ya kujikimu, na kwa upande mwingine upendeleo wa waziwazi unaotolewa kwa watu wenye uwezo wa kifedha hususan wale watokao nje ya vijiji vyao ambao huvuna maliasili na baoanuai yake kwa minajiri ya kujitengenezea fedha na faida kubwa na si kujikimu kama ilivyo kwa wanavijiji.

Licha ya kutoa maoni yao juu ya taratibu, utafiti ulibaini kuwa watu wengi hawazifahamu vyema taratibu mbalimbali za usimamizi, utunzaji na uvunaji wa maliasili za baoanuai, na kama taratibu hizo zilikuwa na manufaa kwao. Katika suala hili waliotoa maoni walionesha kutozijua taratibu mbalimbali zinazosimamia baoanuai mbalimbali. sehemu ndogo sana ya wananchi, yapata asilimia 9.3 ndio ilionesha kuzifahamu taratibu hizo na zaidi ya asilimia 90 walionesha kutozifahamu kabisa taratibu hizo. Kwa hivyo kuridhika au kutoridhika kwao kunatokana zaidi na mahusiano yao na maafisa hifadhi na ufahamu wao wa namna masuala ya usimamizi na uvunaji maliasili yanavyofanyika.

Endelea Uk.5

# Bunga Bongo - Nishati Uoto

MBEZI GARDEN HOTEL - DAR ES SALAAM, 29/02/2008 - 3.15 USIKU

Ijumaa ya tarehe 29 Februari 2008 usiku wa kuamkia Jumamosi tarehe 1 Machi 2008 wanachama, marafiki na wakereketwa wa Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi - HAKIARDHI, walikuwa na Bonga Bongo juu ya suala la Nishati uoto. Suala la Nishati uoto lilichaguliwa kuwa mada kuu ya mjadala kutangulia Mkutano Mkuu wa HAKIARDHI kwa sababu athari za mipango na miradi ya nishati uoto zimeanza kuonekana mapema, wakati hata miradi yenyewe inayokusudiwa kuanzishwa haijakamilika. Yafuatayo ni baadhi ya majadiliano yaliyofuatia mada ya uchokozaji fikra iliyowasilishwa na Ndugu Yefred Myenzi.



**Pius Magai Manyama**
Huko nyuma tuliwahi kuambiwa ... itatengenezwa gari itakayotumia maji,.... sasa tunaambiwa mazao yazalishe nishati, ... chakula hiki kidogo itakuwaje! Ingekuwa mkonge tungeelewa... lakini kusema sehemu ya chakula... hapana! Watu walio wengi hawafahamu suala hili.... viongozi wetu uelewa wao mdogo, ni bwana ndio! Tujiandae kabla hali haijawa mbaya, tukatae suala hili kwa nguvu zote. Tunahitaji chakula!



**Talaka Nyanja**
Hawa viongozi wetu wana elimu ya darasani, lakini hawana elimu ya kusoma kitu... mengi yanatokea hapa kwetu yenye madhara, lakini wao wenyewe wanakubali... madhara si yatatupata sote? Nchi zetu zitakombolewa na wanaharakati na sio viongozi. Wao wametanguliza matumbo... kutawala sio kuwa una akili kuliko watu wote.... kutawala sio kuwa na upeo ... wapo wananchi wenye upeo kuliko hata viongozi.



**Martha Sumaye**
Nimesikiliza, nimeumia, nimeumwa, hata hospitali haiwezi kunisaidia .... Ndio! Kama tumeamua kuumia kwa ajili ya wananchi na kutetea haki zetu hakuna kitakachoshindikana ... Nyerere alikuwa mwenyewe, mkombozi, leo mbona sisi tuko wengi, hoja ni mbinu, si wingi, si pesa! Hivi kuna mwanaume akitaka kukuoa atakuambia atakutesa?... hakuna! ni mbinu tu... tukubali maumivu, tujiweke tayari, tuelekeze nguvu zetu kutetea na kufia haki zetu. Ukifia haki ni vyema sana... mimi siogopi kufa kwa ajili ya haki.



**Rehema Mfaume**
Chanzo cha utajiri wa hao wafadhili ni nini hasa? Kihistoria wao ni wataalamu sana ... viwanda vyao vinacheua na takataka zake wanatafuta pa kuzitupia. Walianza hivi hivi na lelemama wimbo tunaotaka kuimba... hatimaye tukawa magogo... tukitaka kufika juu si kupinga...tuikubali hiyo tekinolojia, tufanye kama hao. Muhimu tujue madhara yake. Sisi leo tunapigiwa hodi na hii tekinolojía mpya basi tuipokee ... wanataka hapa - nchi ya amani, nchi ya utulivu ... wanataka wachukue chao mapema kabla hatujashtuka ... watuachie madhara ... lakini mbona tunalima! Mpunga, mahindi yanayolimwa kwa ngwamba... yatauzwa, pamoja na njaa zetu ... tutauza. Jamani tutafute njia mbadala... shida ni vitendea kazi, watu wazalishe ziada, wale na wauze kwa hao wa mafuta.



**Abdallah Matata**
Wanazalisha haya ili wa-Afrika wawe na njaa. Ukiwa na njaa ni rahisi kukutawala. Ukiwa na uchumi mzuri si rahisi kutawaliwa....


lengo kubwa la hawa wa nchi tajiri ni kutumia rasilimali za Afrika kwa ajili ya maendeleo yao... lengo lingine ni kushika nchi za mashariki ya kati... huu ni mkakati wa wao kuendelea kuitawala dunia. Bush kaja hapa, katusaidia, wale hawasaidii kwa hasara, leo wanatoa Shs 71 kesho wanachuma Shs.700.



**Mzee Emilian Jaka**
Mtu ukiwa fukara inachangia hata kufa mapema. Mimi nadhani lazima kuikabili serikali na hakuna njia ya kuikabili serikali bila kuungana pamoja... ndugu zangu hatuwezi hata kuweka mkakati? Tunashindwa kupata haki zetu sababu ya woga ukijiamini utaweza.. tutafute swala la kuwakata makali hawa viongozi. Je, tunapoongelea jambo litafika?, litawagusa?... tuwaite wahusika, wawepo hapa pamoja nasi watusikie. Mfano wa Delta, wakapinga mradi ule kwa nguvu zote, kiko wapi! mradi haupo tena... Tuitane, haitoshi kusema, tutende.



**Samuel Seya Qawoga**
Huenda huu ndio ukawa msaada wetu wa kujitoa katika umasikini... Katiba inaahidi kulinda ustawi wa wananchi. Kweli serikali inafanya hili, mimi nina mashaka. Hii nishati uoto itatusaidia? ni miradi mingapi imefanyika na hakuna kilichotokea? Tazama miradi ya ngano... tumefaidikaje sisi? Tutaporwa ardhi, na kupata maradhi mengine. Hatuna chakula, ni lini tutazalisha chakula cha kutosha na ziada?



**Bw. Said Mtambo**
Miradi hii ilianza zamani. Tulihamasisha tupande mibono, kwa ajili ya mafuta ya kula. Mibono

Endelea Uk.8

# Ubinafsishaji wa Baoanuai

Inatoka uk. 3



*Mganga wa tiba asilia wa Tangabwa Bongo mizizi akiwaonyesha watafiti baadhi ya dawa anazotumia katika utafiti wa dawa za Ukimwi*

Hatua Mbalimbali za Ulinzi na Uhifadhi wa Baoanuai

Aidha wananchi hawaridhishwi na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili kulinda baoanuai. Hatua hizo kama zilivyobainishwa na wananchi wenyewe ni pamoja na utwaaji wa ardhi. Zaidi ya watu Asilimia 66% miongoni mwa waliotoa maoni yao walionyesha kukerwa na utwaaji wa ardhi zao kwa ajili ya kuhifadhi baoanuai. Njia nyingine zilizotajwa kutumika kuhifadhi baoanuai, hususan maeneo yenye misitu ni pamoja na uhifadhi wa misitu na uzuiaji wa wananchi kuingia katika hifadhi. Utwaaji wa ardhi kwa ajili ya ama kuongeza eneo la hifadhi au kuanzisha hifadhi limekuwa ni jambo linaloendelea na limekuwa chanzo cha migogoro na mivutano baina ya wananchi na mamlaka mbalimbali za serikali. Wananchi hawaoneshi kuridhika na namna migogoro hiyo inavyotatuliwa. Mara nyingi pindi migogoro ya aina hiyo inapozuka wananchi wamekuwa wakihamishwa kwa nguvu. Watu wa Kazimzumbwi bado wanakumbuka, hata wakati wa kufanya utafiti huu, jinsi walivyochomewa nyumba zao na kuhamishwa kwa nguvu kwenye eneo lililodaiwa kuwa wamevamia.

## Chombo gani wangependelea Kisimamie?

Kuhusu mamlaka ipi wangependa ipewe jukumu la usimamizi wa maliasili katika maeneo ya vijiji, zaidi ya 54% ya waliotoa maoni wangependelea Mamlaka za Serikali za vijiji zipewe jukumu la usimamizi wa maliasili. Zaidi ya 25% walipendekeza usimamizi uendelee kuwa chini ya serikali kuu na kiasi cha 14% ya waliotoa maoni walipendekeza kubinafsisha usimamizi huo na kati ya kiasi hicho 9% walipendekeza yapewe makampuni ya nje na 4.7% makampuni ya hapa nchini. Waliopendekeza mamlaka za serikali za viji walibainisha kuwa vyombo vinavyosimamia na taratibu zinazotumika kulinda maliasili na baoanuai yake hauna manufaa kwao. Katika suala la kama wananufaika na hatua na taratibu mbalimbali za uvunaji, wananchi zaidi ya 86% walionesha kuwa taratibu hizo zina manufaa kidogo sana kwao na 10% walionesha kuwa zina manufaa makubwa. Kiasi cha asilimia 2.7 kilionyesha kuwa hazina manufaa kabisa. Waliotoa maoni ya kuweka usimamizi wa maliasili chini ya mamlaka za vijiji wanahisi kuwa mamlaka hizo zitazingatia zaidi maslahi ya wanavijiji badala ya wageni na watu kutoka mijini.

Majibu ya suala hili yanaoana na yale ya suala la ni wapi maliasili inayovunwa iendako? Kuna hisia miongoni mwa watu waliotoa maoni kuwa, kama ilivyo kwa maeneo mengine ya rasilimali za nchi, uvunaji wa baoanuai pia unapendelea watu wa nje na wale wa mijini na si watu wa kawaida hususan wale wa vijijini. Mathalani kwenye majibu juu ya swali ni wapi mavuno ya maliasili hupelekwa wengi walibainisha kuwa mavuno hupelekwa zaidi mijini na nje ya nchi. Zaidi ya asilimia 33 ya waliohojiwa walieleza kuwa mazao hayo hupelekwa nchi za nje na asilimia 52 walitaja maeneo ya miji kuwa ndiko mazao hayo yanakokwenda. Asilimia 1.4 tu ndio waliotaja maeneo mengine ikiwa ni pamoja na matumizi katika maeneo ya vijijini. Hisia zao zinaoana pia na taarifa mbalimbali ambazo zimekuwa zikichapishwa na vyombo vya habari juu ya usafirishaji wa magogo nje ya nchi kinyume cha taratibu. Aidha katika baadhi ya maliasili zinazovunwa na kusafirishwa ni pamoja na wadudu, nyoka, na mimea mbalimbali yenye uwezo wa kutibu magonjwa mbalimbali. Haya yanafanyika japo hayapati nafasi kubwa katika vyombo vya habari.

# Uporaji wa rasilimali za maskini kwa mwega wa maslahi ya Taifa




Na Evaristo Haulle

Toka wakati wa ukoloni jamii za ki-Tanzania kwa nyakati mbalimbali zimekuwa zikiporwa rasilimali zao kwa visingizio mbalimbali. Toka uhuru upatikane uporaji huo umekuwa ukifanyika kwa sababu mbalimbali ikiwemo 'maslahi ya umma au taifa'. Ni kwa 'maslahi ya umma' Wa-barbaig wa kule Hanang waliondoshwa kwenye ardhi yao kupisha mashamba makubwa ya ngano, na wao wakiachwa kutangatanga na mifugo yao wakitafuta sehemu nyingine ya kujihifadhi na kujikimu.

Katika Mkoa wa Tanga, ardhi ya wenyeji, pia imeporwa na imeendelea kuporwa kwa miongo kadhaa kwa sababu mbalimbali. Mnamo mwaka 1957 ardhi ya wenyeji ilichukuliwa katika eneo la Amani Wilayani Muheza kwa ajili ya kupisha uanzishwaji Kituo cha Utafiti Amani ("Royal Botanical Garden"). Aidha mwaka 1997 Bunge lilipitisha sheria ya kuanzisha Hifadhi ya Asili ya Amani (Amani Nature Reserve) . Uanzishwaji wa Hifadhi hiyo umefuatiwa na wananchi kuondolewa katika ardhi inayotakiwa kwa ajili ya hifadhi. Utekelezaji wa uamuzi huu kati ya 2002 - 2005 umeathiri wananchi wengi katika tarafa ya Amani na sehemu nyingine za Wilaya ya Muheza na Korogwe ambao wamelazimika kuondoka katika ardhi zao. Kufuatia uanzishwaji wa hifadhi na kupora ardhi za wananchi eneo la hifadhi hiyo sasa ni kiasi cha hekta 8,380, eneo ambalo linajumuisha hifadhi sita za vyanzo vya maji zilizokuwa zikijitegemea na vijiji vipatavyo 18.

Kama ilivyo kwa uporaji wowote, sababu na misingi ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa huonekana au kuelezwa kuwa na manufaa kwa umma mzima na wananchi wanaoondolewa. Aidha wananchi huahidiwa kufidiwa mali na ardhi zao. Lakini yote haya huchukua sura tofauti pindi uamuzi unapokuwa unatekelezwa au unapokuwa umeshakamilika utekelezaji wake. Fidia huwa hazilipwi na pale zinapolipwa huwa za kupunja punja. Sura hii ndio pia inajitokeza katika eneo ilipoanzishwa hifadhi hii. Wananchi waliahidiwa fidia kwa mazao yao ambayo ni pamoja na iliki, migomba, na karafuu. Lakini fidia ilipoanza kulipwa ilikuwa kinyume na makubaliano. Mathalani katika vijiji vya Kwezitu na Kwezulu, mahali ambapo mwandishi na mtafiti huyu alitumia muda kujadiliana na wananchi kadhaa, makubaliano ya awali ya fidia kwa shina la iliki yalikuwa Sh. 28,800/=. Kilicholipwa, kwa waliobahatika kulipwa ni 1,500/=. Wananchi wakulima wa iliki hawaoni kuwa walitendewa haki kwa malipo madogo kama hayo haswa ikizingatiwa kwamba huchukua miezi 18 hadi 24 kwa mmea wa iliki kufikia kuanza kuvunwa na shina moja la iliki lina uwezo wa kuzalisha robo debe kwa mwaka (sawa na kilo 5) ambapo kilo moja ya iliki huuzwa kati ya Tsh.3,000 na 4,500/=. Hivyo shina moja huzalisha kati ya Tsh. 15,000 na 22,500/=. Hali hii ndivyo ilivyo kwa fidia ya mazao kama vile migomba na karafuu ambazo zilifidiwa kwa shilingi 8,000/= badala ya 20,000/=, na mikarafuu sh. 2,000/= badala ya sh. 25,000/= zilizoahidiwa katika makubaliano. Kwa hivyo katika uanzishwaji wa hifadhi asilia ya Amani wananchi sio tu walipoteza ardhi lakini pia walilipwa fidia ndogo sana. Kuna tofauti kidogo kwa wananchi wa vijiji vya IBC-Msasa Kata ya Kisiwani na Ingawaje kilichoko kata ya Zilai, hawa walienda Mahakamani kupinga fidia iliyokuwa ilipwe kwao.

Endelea Uk.7



*Mojawapo ya hifadhi ya msitu wa tao la mashariki ulioko milima ya Usambara yenye baoanuai nyingi*

# Uporaji wa rasilimali za maskini

Inatoka uk. 6

Sababu za kuanzisha Hifadhi ya Asili ya Amani ni za kukuza na kuhifadhi mazingira na baoanuai yake. Hakuna asiyetambua umuhimu wa suala la hifadhi bora manufaa yanayotokana na shughuli mpya ziwe za uhifadhi au uwekezaji mwingine katika maeneo hayo ambayo wananchi huyapata mara nyingi ni kiasi



*Uporaji wa Ardhi nzuri kama hii huathiri maisha ya wananchi*

ya mazingira. Lakini hili halihalalishi dhuluma na udunishaji wa utu na maisha ya watu kwa kutozitambua haki zao, kuzididimiza jitihada zao, na kuuharibu ustawi ambao wanakuwa wameufikia kama watu au jamii kutokana na uzalishaji ambao wamekuwa wakiufanya.

Hali kama hii imekuwa ikwapata wananchi wengi wanaoishi katika maeneo yaliyojaliwa kuwa na rasilimali asilia nyingi kama ardhi yenye rutuba, wanyamapori, madini, misitu na hata wadudu. Badala ya kuwashirikisha wananchi katika maamuzi juu ya mustakabali wa maliasili hizo, kinyume chake hutokea pale wanapotimuliwa na kuambulia fidia isiyoendana na thamani halisi ya maendeleo, ustawi, utu na maisha yao kwa ujumla. Jambo linalofanyika kwa manufaa ya umma linafaa kuamuliwa na umma na wala si wachache kwa manufaa ya wachache. Hata kidogo sana kulinganisha na mapato halisi ya shughuli husika. Ipo mifano halisi ya vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi kama vile Kwezitu ambacho hupata gawio la mapato yatokanayo na hifadhi la sh. 105,778/= kwa mwaka? kiasi ambacho ni kidogo mno katika kusaidia mabadiliko ya msingi ya maisha ya wanakijiji wapatao 2400, ambao tayari wamedhoofishwa na usumbufu, na hasara nyingi walizozipata kwa kuondoshwa kwenye ardhi zao. Wakati wananchi wanazuiwa kutumia rasilimali za hifadhi wahifadhi wanawaruhusu watu wengine kuvuna magogo na viumbe wengine kama nyoka kwa maslahi binafsi na si ya umma au taifa. Ndio maana wananchi sehemu mbalimbali wanaendelea kutilia mashaka sababu zinazotolewa kila hifadhi mpya inapoanzishwa na hutoa upinzani dhidi ya uanzishwaji wake.

## MAONI

***Dude hili la nishati za mimea litupitie mbali jamani***

*Nimesikia katika vyombo vya habari kuwa hivi sasa nchi za Ulaya na Marekani pamoja zimekuja na kampeni kabambe ya kutumia mazao ya chakula kutengeza mafuta ya magari na mitambo mbalimbali. Kwakweli mwanzoni sikuwa naelewa na sikufikiri kama hayo mambo yanaweza yakatuhusu sisi wa-Tanzania hasa wanavijiji huku mbali. Lakini hivi juzi juzi nimeoana katika TV mtaalamu mmoja wa shirika la Hakiardhi akieleza kuwa wawekezaji kutoka nchi hizo tayari wako nchini na wanatafuta ardhi vijijini kwaajili ya kulima mijatropha na miwa ili kutengeneza mafuta.*

*Nionavyo mimi, hapo ndipo kifo chetu kilipo. Watanzania wengi tunategemea ardhi kulima tupate chakula na kidogo tuuze tununue nguo na watoto waende shule. Leo hii ardhi ikitumika kuzalisha hiyo jatropha, chakula kitatoka wapi? Na isitoshe, nikasikia tayari wawekezaji wanawahi kuchukua sehemu za mabonde yenye rutuba kama Rufiji, Usangu, Kilombero na Ruaha pamoja na maeneo yanayozalisha chakula huko Mpanda, Tanga, Mtwara na Ruvuma. Kama hali ndiyo hiyo nina uhakika muda si mrefu tutakuwa na njaa isiyokwisha kwani hata chakula chetu wenyewe hatutaweza kulima wala kununua maana hata bei sharti ziwe juu kwavile kitakuwa haba. Nawashauri watu wa Shirika la Hakiardhi waongeze elimu vijijini ili wananchi wayajue zaidi mambo hayo na wachukue tahadhari.*

*Mimi nachukulia nishati ya mimea kama dude linalokuja kutuangamiza kwa kuchukua ardhi yetu, chakula chetu, maji yetu ya kumwagilia mazao na bei ya mazao yetu. Ni heri likapita mbali nasi ili tusife kwa njaa wakati uwezo wa kujikimu kwa ardhi aliyotupa mwenyezi Mungu tunao.*

*Shukuru Kikole*
*Kilosa*
*Morogoro*

***Ndugu wapendwa wa Hakiardhi,***
*Napenda kuwasalimu sana na kuwapa pole ya kazi kwa kuelimisha umma wa wa-Tanzania juu ya haki zao za ardhi. Sisi wananchi wa Hanang kweli tulielimika sana juu ya mafunzo yenu na mengi yametusaidia sana katika shughuli zetu za kila siku za harakati za kutafuta haki. Hata hivyo, tunaomba yale majarida ya elimu ya Ardhi ni Uhai pamoja na Kalenda zenu zitufikie kwani watu wengi wamekuwa wakiulizia sana. Mimi nimefikia hatua ya kutoa nakala na kuwagawia wale wanaohitaji ili angalau wananchi wengi zaidi waweze kupata elimu hii. Nitashukuru sana kama mtatupatia tena majarida na kalenda kulingana na mahitaji yetu. Kwa sasa angalau tunaomba nakala miatano (500).*

*Martha Laurent*
*Kijiji cha Galangal*
*Hanang*

***Ndugu wahusika wa Hakiardhi,***
*Mimi niliwahi kushiriki katika kongamano la taifa la ardhi liliofanyika kule Baraza la Maaskofu Katoliki Kurasini Dar es salaam mwaka 2005 na tangu hapo sijawahi alikwa tena. Lakini ninapenda kweli kushiriki mijadala kama ile kwani ilinifungua sana uelewa wangu wa masuala ya ardhi. Wakati ule huku kwetu tulikuwa tunaona kama ardhi haina maana lakini sasa wameanza kuja wawekezaji wanatafuta ardhi kwa ajili ya kupanda miti na ardhi sasa inaanza kuonekana ina maana. Je lini tena mtafanya kongamani kama lile? Au mmeacha siku hizi kuyafanya. Naomba sana niweze kushiriki kama yapo kwani kuna mambo mengi napenda kuwashirikisha na wengine pia kujifunza kutoka kwao.*

*Asante kama mtanijibu.*

*Ronico Elias*
*Kiwalamo Kilolo*
*Iringa*

# Bunga Bongo - Nishati Uoto

Inatoka uk. 4 tunaifahamu, lakini tunaipanda uani. Wahindi fulani walikuja, wakasema wao wataleta soko, tukawakaribisha baadae wakaondoka. Hili la sasa hivi ndio hivyo, wenzetu wa EIA (Environmental Impact Assessment) wametueleza madhara, inaelekea wananchi hawakushirikishwa kikamilifu, hawakupewa taarifa za kutosha, wananchi hawana elimu hii. Je, Taasisi yetu ina nafasi gani katika kupeleka hili kwa wananchi wengi zaidi na serikalini?



**Subira Kibiga**
Hawa wenzetu wanae mfariji wa kuchezea kamari. Wewe unayecheza nao kamari mtaji wako mdogo huwezi kufikia huo mchezo. Nishati hiyo siyo ya kuendeshea gari yako Kamata, wala sio yangu, ni yake, na ya Bush, kule kwao. Wanaobuni hiyo miradi ni wenzetu, makuwadi, wanatuchezea shere... hawana uchungu na hii nchi... uroho umeingia



**Marcelina Charles**
Tunaondoka na nini baada ya mjadala huu? Nini tunafanya kuepusha haya madhara? Watu wanaongea kwa uchungu, wako tayari kufa siyo kufariki. Sasa tuweke kitu cha pamoja ili wanachama tujue nini cha kufanya, nini wajibu wetu?



**Bertha Koda**
Tunafanya nini? Martha alitusaidia, tutafute mkakati mzuri na madhubuti wa kuzuia hili... tuwe na mkakati wa kisayansi ili tuondoke hapo. Watakuja na mbinu nyingi- mfano wa mbaa, wapo waliokula, wakatoa ardhi, na wapo waliokula na wakakataa kutoa ardhi. Hili suala la kujilinganisha na wamarekani na waingereza hivi ndivyo tunakotaka kwenda huko? Tutengeneza dira yetu... tufanye yale yaliyo ndani ya mpango wa Taasisi. Taasisi itutengenezee ka-utaratibu ili tujue.



**Alquin Senga**
Vilianza viwanda, tukaambiwa viwanda vikiuzwa tutaendelea, serikali itapata faida. Kati ya Viwanda 450 viwili tu vinapigiwa kelele - Sigara na Bia. Viwanda vingine vikachukuliwa vyuma vikauzwa, chuma kikawa chakavu kikauzwa. Tumeuza! Leo tunalia ajira hakuna, malipo kidogo... leo wanarudi, wanafuata ardhi yetu. Tuliambiwa ukitaka kuendelea ardhi, siasa safi, uongozi bora, na watu, sasa leo anga limeenda, ardhi wanachukua, Madini yameenda...tumebaki na nini? Wafanyakazi na wakulima tushirikiane kuwa 'machizi' tukomboe nchi yetu.



**Mzee Ally Abbas**
... nawauliza tuko serious na ukombozi wa taifa letu.... hatuwezi kukomboa kwa maneno bila vitendo. Tutaondoka hapa, na makaratasi haya, tutafungia vitumbua, tutaishia hapo. Waliokomboa nchi hii walisema wakatenda. Mkoloni akaondoka lakini mkoloni aliondoka akitaka awe na watu wake... hayo tunayoyasema yamefika wapi? Vyama vya siasa, vyama vya wafanyakazi havina mwamko. Watu tunatafuta umeme tunafikiria kibatari. Tunataka Azimio, nini tutafanya ili kukomboa nchi yetu. Lazima tuunganishe nguvu, vyama vya siasa na taasisi zingine. Tutakapofanya mkutano mwingine tuwaalike wengine. Hii sio nchi ya HAKIARDHI peke yake.



**Bashiru Ally**
Katika suala hili tumegawanyika vipande. Hili swala linaongozwa na Rais, alisema katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi. Anaona kama ukombozi ndani ya mashirika haya pia tumegawanyika, wanatafuta mafuta ya koroboi. Ni suala lenye ugumu wake. HAKIARDHI kama Taasisi angalau imejitahidi kuliweka mahala suala hili, tusikate tamaa, tumepata taarifa kidogo. Tupewe taarifa, Shinyanga, huko ndiko kwenyewe, Madini - kampuni zinasaidia kilimo cha mibono. Huko walikokula mbaa, Rais alikwenda eneo hilo, akiwa amevalia T-Shirt ya mwekezaji - SEKAB, ni suala gumu. Tunachohitaji sisi tulio kwenye utafiti ni taarifa! zitatusaida kujenga hoja. Kuna watu wengine wanaanza kuingia, SUA kuna wataalam wanafanya utafiti wa kusaidia kilimo, pale Chuo Kikuu cha Dar es salaam, kuna utafiti unaendelea, sijui utatoa taarifa gani, Tunahitaji maandalizi, tunaweza kuwa waandishi wa ukombozi wa suala hili. Vijana si woga, tukubali ugumu, tunahitaji kujipanga.

**Nyongeza:** Mjadala ulikuwa mrefu na uligusa hisia za washiriki. Suala walilokuwa wakijadilina hivi sasa ni suala lililozua mjadala mkubwa duniani kote hasa kufuatia ongezeko la bei za chakula duniani kote, ongezeko linalohusishwa na matumizi ya chakula kwa ajili ya kutengeneza nishati. Hivi karibuni, alipotembelea nchini Uchina Rais wa Jamhuri alinukuliwa kuchukua msimamo mkali dhidi ya matumizi ya chakula kwa ajili ya mafuta. Tunakaribisha maoni na michango mbalimbali ili kuendeleza mjadala juu ya suala hili muhimu katika maisha ya watu wengi, hasa mafakiri. (Mhariri).

*Karibuni sana katika Semina za kila mwezi kuhusu maswala ya Ardhi zinazofanyika kwenye ofisi zetu za Haki Ardhi.*

*Na Baha Bernard*



# Hifadhi ya Mali asili Bahari Uzoefu wa wananchi wa Mafia

KISIWA cha Mafia ni mojawapo ya Wilaya sita za Mkoa wa Pwani. Kinapakana na Dar es Salaam kwa upande wa Kusini na kiko Kilometa 120 toka Dar es Salaam na takribani kilometa 20 toka pwani ya Mashariki ya delta ya Rufiji. Kisiwa mama cha Mafia kina kadiri ya urefu wa kilometa 48 na upana wa kilomita 17. Kuna visiwa vingine vidogo vidogo magharibi na kusini mwa Kisiwa hiki. Katika kisiwa hiki ndipo iliko hifadhi kubwa ya baharini (Mafia Island Marine Park). Hifadhi hii ina ukubwa wa kilometa za mraba 822. Hifadhi inahusisha visiwa vya Chole, Juani, Jibondo na Bwejuu na visiwa vidogo vidogo visivyokaliwa na binaadamu. Kihistoria, wazo la uanzishwaji wa hifadhi za bahari lilianza mara tu baada ya Tanzania (Tanganyika) kujipatia uhuru mnamo mwaka 1961. Kwa sababu mbalimbali hili halikuweza kufanyika hadi kabla ya mwaka 1995. Mpango wa hifadhi ulihusisha eneo la pwani ya bahari ya Hindi lenye ukubwa wa km 800. Maeneo tengefu ya hifadhi bahari kwa upande wa Tanzania bara ni maeneo yote yaliyotengwa kwa mjibu wa sheria ya Hifadhi za bahari na maeneo tengefu namba 29 ya 1994. Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia imeundwa na inasimamiwa kwa mjibu wa sheria hii.



*Aina mojawapo ya samaki ayesadikiwa kuwa katika hatari ya kupotea katika kisiwa cha Mafia. Uvuvi haramu umechangia samaki hawa kupotea*

**Wavuvi na Hifadhi.**

Shughuli kubwa za wakazi wa Mafia ni Uvuvi na kilimo. Kati ya makundi haya mawili kundi la wavuvi wameathirika zaidi na uamuzi wa kuanzisha hifadhi katika kisiwa cha Mafia. Aina ya hifadhi na utaratibu unaowekwa unazuia shughuli za uvuvi wa aina yoyote isipokuwa katika maeneo yaliyotengwa maalum mbali na mazalia ya samaki na matumbawe ikiwamo kupiga marufuku uvuvi wa baadhi ya viumbe bahari. Kama ilivyo kwa maeneo mengi ya Pwani na visiwa, kisiwa cha Mafia nacho pia kilikabiliwa na tatizo la uvuvi haramu na mojawapo ya malengo ya kuanzishwa hifadhi mbali na kuhakikisha ulinzi na maendeleo ya viumbe bahari ilikuwa pia ni kukabiliana na wavuvi ama uvuvi haramu. Kwa mujibu wa Idara ya uvuvi katika halmashauri ya wilaya ya Mafia kuna ongezeko la samaki na viumbe bahari toka kuanzishwa kwa hifadhi. Hii inatokana pia na kupungua kwa kiasi kikubwa kwa uvuvi haramu katika eneo la hifadhi. Ongezeko hili la samaki na viumbe bahari kwa upande wa wananchi wavuvi katika maeneo haya unapokewa kwa hisia tofauti wengi wakionyesha kutoridhishwa na mbinu za uhifadhi zinazotumika. Wakati ambao idara na watendaji wa hifadhi wanafurahia ongezeko la samaki wavuvi wadogo wanaotumia vyombo na zana duni za uvuvi na wanaolazimika kwenda kuvua katika maeneo yaliyotengwa maalum kwa ajili ya uvuvi wanalalamika juu ya kutopata samaki wa kutosha katika maeneo hayo. Kwa upande wa visiwa vilivyomo ndani ya hifadhi hali ni mbaya zaidi hasa ikizingatiwa kwamba tofauti na wavuvi katika maeneo mengine hawa hutegemea kwa kiasi kikubwa uvuvi kuendesha maisha yao.

Kisiwa kama cha Jibondo ambacho ardhi yake haifai kwa kilimo kwa sababu ni mwamba tegemeo kubwa la wakazi wake ni uvuvi. Kabla ya uanzishwaji wa hifadhi kulikuwa na ushirikishwaji wa wananchi watakaoathirika na hifadhi hii katika vijiji 14, kwa mujibu wa Idara ya uvuvi hali ilivyokuwa sasa tofauti na wakati huo ni kwamba kuna upinzani dhidi ya malengo ya programu ya hifadhi hasa kutoka kwa kundi la vijana ambao hawakuwapo wakati wa kampeni za mwanzo za Endelea Uk.11

# Kona ya Sheria

## Cheti cha Hatimiliki ya Kimila

Katika toleo lililopita makala ya Kona hii ilizungumzia maana ya hatimiliki ya kimila na upatikanaji wake. Kwa ufupi, hatimiliki ya ardhi ya kimila ni aina mojawapo ya umiliki wa ardhi inayotambuliwa kisheria ambapo mmiliki anakuwa na haki juu ya ardhi anayotumia kutokana na uasili wake katika eneo hilo, kurithi kwa wazazi wake, kupewa zawadi au kugawiwa na serikali ya kijiji/mtaa.

Leo tutazungumzia kuhusu cheti cha hatimiliki ya kimila na upatikanaji wake. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya 1999 fungu la 7 (7) cheti hiki kinafafanuliwa kuwa ni hati anayopewa mmiliki wa ardhi kwa njia ya kimila hasa baada ya kijiji anapoishi mmiliki huyo kubainishwa mipaka yake na kupewa cheti cha ardhi cha kijiji. Cheti cha ardhi cha kijiji ni zao la sheria ya ardhi ya vijiji ambacho hutolewa kwa Halmashauri ya Kijiji kuonyesha nguvu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji husika. Kutolewa kwa cheti hiki kumefuta hatimiliki za ardhi ya kijiji ambazo baadhi ya vijiji viliwahi kupewa tangu miaka ya 1970's. Hivyo basi kila Halmashauri inayokidhi sifa za kupata cheti cha ardhi cha kijiji, itakabidhiwa vyeti vya hatiliki za kimila ili kuzigawa kwa mwanakijiji mmojawapo anayemiliki ardhi kimila. Kabla ya utaratibu huu, Halmashauri ya Kijiji isingeweze kumilikishwa hatimiliki za kimila kwa vile zenyewe (Halmashauri) ndizo zilizokuwa zikimiliki ardhi kwa hatimiliki ya ardhi ya kijiji.

Cheti cha ardhi cha kijiji, kwa mujibu wa fungu la 7 (a) kinapaswa kutolewa kwa amri ya Rais kwa Halmashauri ya Kijiji husika, na kitatolewa tu endapo kijiji husika hakina migogoro ya mipaka dhidi ya kijiji au mamlaka nyingine na mipaka yake kuwa imebainishwa ili kuendana na mipaka ya kiutawala kama ilivyoainishwa katika cheti cha kijiji. Cheti cha kijiji ni usajili wa vijiji tofauti na cheti cha ardhi cha kijiji ambacho hutolewa na Kamishna wa Ardhi kwa amri ya Rais.

Cheti cha hatimiliki ya ardhi ya kimila kinapaswa kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu wa Halmashauri ya Kijiji husika na kutiwa saini na kuwekwa alama na mmiliki wa hati hiyo chini ya ukurasa wa cheti. Pia cheti hiki kitatiwa saini kuwekwa lakiri na kusajiliwa na Afisa Ardhi wa Wilaya ambayo kijiji husika kimo.

Licha ya kuwa utolewaji wa cheti cha ardhi cha kijiji pamoja na kile cha hatimiliki ya ardhi ya kimila unaonekana kama hatua muhimu katika kukabiliana na matatizo sugu kwenye mfumo wa milki ya ardhi nchini, bado kuna changamoto muhimu ambazo ni vema zikajadiliwa kwa umakini unaostahili. Kwanza, ni ukweli usiofichika kuwa vijiji vingi vya Tanzania havina mipaka bayana na hiyo imekuwa moja ya sababu kubwa ya kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara na kwa mantiki hiyo havina sifa ya kupata cheti cha ardhi cha kijiji hadi mipaka yake ibainishwe. Hata vile ambavyo viliwahi kupimwa, mipaka yake ina utata na bado imekuwa kiini cha mapigano ya mara kwa mara. Mfano hai ni vijiji vya Tarafa ya Sale na vile vya tarafa ya Liliondo Wilaya ya Ngorongoro ambavyo licha ya kupimwa miaka ya 80 chini ya mradi wa ADO, mipaka yake haikubaliki na wanavijiji na ndio kiini cha mapigano ya Batemi wa Kisonjo na Morani wa Kimasai ambayo yamedumu kwa takribani miongo mitatu sasa. Hadi pale vijiji hivyo vitakapokubaliana mipaka ndipo vitakidhi sifa ya kupata cheti cha ardhi cha kila kijiji na ndipo vyeti vya hatimiliki za kimila vitakapoanza kutolewa. Sasa huu ni mfano mmoja tu katika mingi iliyotapakaa nchi nzima. Pili, mchakato wa upatikana vyeti hivyo ni mgumu na wa gharama. Si rahisi wanakijiji kuanzisha utaratibu wa kupima vijiji vyao bila ya halmashauri za wilaya na halmashauri nyingi zimeshindwa kutekeleza jukumu hilo kwa hilo kwavile hazina vitendea kazi wala rasilimali watu za kutosha. Gharama ya kupata cheti cha ardhi ikiwa ni pamoja na uhifadhi wake zimekadiriwa na kufikia hadi shilingi laki nane. Je, ni vijiji vingapi na halmashauri ngapi za Wilaya ziko tayari kukamilisha mchakato huo kwa wakati na kwa ufanisi?

Tatu elimu kuhusu upatikanaji wa vyeti hivyo na umuhimu wake bado haujawafikia siyo tu wananchi bali hata watendaji katika ngazi za Halmashauri za Wilaya ambao ndio wenye majukumu ya kuwezesha upatikanaji wa vyeti hivyo muhimu. Je katika mazingira hayo, ni vema kuhamasisha wananchi kutumia ardhi yao kama dhamana ya mikopo katika taasisi za kifedha kabla elimu hii haijawafikia? Hatimiliki za kimila ni muhimu zikatolewa kwa wanavijiji lakini katika mazingira ambayo wameandaliwa kikamilifu ili wawe washiriki kamili katika taratibu mbalimbali zinazohusu mfumo wa milki ya ardhi uliopo badala ya kuwa wahanga wa mabadiliko wasiyoyajua.

# Hifadhi ya Mali asili Bahari:...

Inatoka uk. 9

uanzishwaji wa hifadhi. Ikumbukwe kwamba wakati hifadhi inaanzishwa wakazi wa Kisiwa cha Jibondo waliahidiwa ahadi mbalimbali ili waachane na shughuli za uvuvi katika maeneo yaliyotengwa isipokuwa katika maeneo ambayo uvuvi umeruhusiwa. Pia matumizi ya matumbawe kwa ajili ya ujenzi nayo yalipigwa marufuku. Ili waweze kuendeleza maisha yao waliahidiwa kupatiwa zana mbalimbali za uvuvi ikiwa ni pamoja na vifaa na malighafi mbadala kwa ajili ya ujenzi. Mfuko wa hifadhi ya mazingira asilia duniani (WWF) ulikuwa msitari wa mbele katika kuhimiza mabadiliko kwa upande wa wakazi wa kisiwa cha Mafia hasa katika kupiga vita uvuvi haramu wa kutumia baruti. Taarifa zinaonyesha kuwa walifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika hili lakini tatizo likawa katika upatikanaji endelevu wa vifaa vya ujenzi hasa ikizingatiwa kwamba wakazi hawa katika visiwa vya Mafia toka enzi za mababu wamekuwa wakitumia matumbawe kutengeneza matofali ama kama malighafi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi.

Maofisa katika Idara ya uvuvi wanatofautiana kuhusu chanzo cha wakazi wa visiwa cha Jibondo kuonyesha upinzani dhidi ya Mpango wa Hifadhi bahari ya Mafia. Baadhi wadhani kwamba chanzo hasa cha tatizo ni kundi la vijana ambao wakati makubaliano yanafikiwa kuhusu utekelezaji wa malengo ya programu walikuwa bado wadogo au hawajazaliwa hivyo hawaelewi manufaa ya hifadhi. Kundi la pili lina mtazamo kwamba kutotekelezwa kwa makubaliano yaliyofikiwa kati ya WWF kwa upande mmoja na Serikali na Wakazi wa visiwa vilivyoathiriwa ni tatizo na chanzo kikubwa cha upinzani unaojitokeza sasa. Mbali na ugumu wa maisha kwa wakazi wengi wa visiwani ambao tegemeo lao kubwa ni uvuvi, sheria na taratibu zinazotumika katika jitihada za hifadhi hazikujali kabisa kuhusu namna ambavyo jamii hizi zitaendesha maisha. Akiongelea kuhusu hili Msimamizi wa hifadhi anakiri wazi kwamba ni kweli wananchi katika eneo hili wanapata matatizo hasa pale wanapozuiwa kuvua katika maeneo waliyozoea.

Kutokana na matukio haya wakazi wengine katika maeneo ya hifadhi wanapata wakati mgumu katika utekelezaji wa programu ya kuhifadhi bahari. Kuna miradi mbalimbali ya kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kuhifadhi bahari na baoanuai yake katika kisiwa cha Mafia. Kwa vijiji vinavyozunguka eneo la hifadhi, hasa kwa vile vilivyoko katika kisiwa mama, wakazi wake bila shaka hali zao haziwezi kulinganishwa na wakazi wa Jibondo ambao hawategemei sana uvuvi ili kujikimu kimaisha. Katika hali ya namna hii migogoro haiepukiki kwasababu malalamiko ya wananchi hayapewi uzito unaostahili na pengine hupuuzwa tu. Msisitizo katika kuhifadhi bila kujali namna ambavyo wakazi wanaoathirika na maamuzi hayo unaweza kuleta matokeo mabaya kwa jamii kwani kusisitiza ulinzi na hifadhi wa samaki na viumbe wengineo bila kujali masilahi na ustawi wa jamii zinazozunguka na kutegemea rasilimali hizo kama vyanzo vya kipato na kujikimu kimaisha hauwezi kuwa endelevu.

Hivyo basi ni muhimu sana kwa wale wote wanaohusika na uhifadhi wa rasilimali za baoanuai kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika maamuzi juu ya hifadhi na matumizi ya rasilimali hizo. Wakazi katika visiwa vya Mafia wanashuhudia kwamba uvuvi wa kutumia baruti haikuwa jadi yao isipokuwa imeletwa na wavuvi kutoka maeneo mengine hususan Zanzibar. Wao walikuwa na mifumo yao ya ulinzi na uhifadhi ambayo ilikuwa inaheshimiwa. Kwa mfano ilikuwa ni marufuku kuvua samaki katika maeneo ambayo yalihisiwa kuwa ni mazalia ya samaki. Uvuvi katika maeneo maalumu uliruhusiwa tu pale ambapo samaki katika maeneo yaliyokubaliwa kwa uvuvi walikuwa wamepungua sana au kokosekana kabisa. Na ili kuhakiki kwamba haufanyiki uharibifu, aina maalumu tu ya mishipi ndio iliruhusiwa kwa ajili ya kuvua samaki wa kutosha kwa kitoweo. Njia hizi na mbinu mbalimbali za jadi ni muhimu sana zingezingatiwa pia katika kuhakikisha uhifadhi bila kuathiri mfumo wa maisha wa wakazi katika visiwa hivi. Pale inaposhindikana basi waathirika waone faida ya wazi ya uhifadhi kwa maana ya maendeleo ya miundo mbinu na huduma za jamii kama matokeo ya jitihada na kufunga kwao mkanda kuvumilia makali yatokanayo na hifadhi katika maeneo yao.



*Sheria na taratibu zinazotumika katika hifadhi ya Bahari bado hazifahamiki kwa wananchi*

HAKIARDHI ARDHI NI UHAI



*Uwindaji haramu unatishia uwepo endelevu wa wanyama kama hawa*

Anuani/Ofisi
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org

## MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 2. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 3. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 4. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika (Mhariri) |
| 5. | Msukumo na Harakati za Kubadili Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania - *2000* | Ng'wanza Kamata (Mhariri) |
| 6. | Maasai Rights in Ngorongoro, Tanzania - *1998* Kapinga | Issa G. Shivji & Wilbert |
| 7. | Haki za Wamaasai waishio Hifadhi ya Ngorongoro *1999* Kapinga, | Issa G. Shivji, Wilbert |
| 8. | Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania, *1997* | Issa G. Shivji and Wilbert Kapinga (Wahariri) |
| 9. | Ripoti ya Tume ya Rais kuhusu maswala ya Ardhi - *1994* | Wizara ya Ardhi |
| 10. | Reclaiming the Land | Sam Moyo & Paris Yeros |
| 11. | The Silences in the NGO Discourse - Occassional Paper No. 1 May, *2006* | Issa G. Shivji |